NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

9 Mei 2020

Kwa Mabaraza yote ya Kiroho ya Kitaifa

Marafiki wapendwa sana,

Kama ambavyo hadi sasa itakuwa dhahiri kabisa, mwaka wa mwisho wa Mpango wa Miaka Mitano umeleta changamoto za tofauti na zile za miaka minne iliyotangulia. Ulimwengu umenaswa katika nguvu ya ueneaji wa haraka wa virusi ambavyo vimegharimu maelfu kwa maelfu ya maisha na kuvuruga vibaya sana sehemu kubwa ya shughuli za kijamii na za kiuchumi za binadamu. Hata hivyo jumuiya ya Kibahá'i imebakia tulivu na makini na imetenda kwa haraka ili kutimiza matakwa ya haraka yaliyoikabili. Imetafuta njia ili kuhakikisha uendeleaji wa maisha ya kijumuiya, huku pia ikijitahidi kutimiza jukumu lake katika kufikia mahitaji ya kiroho na ya kimwili katika jamii kwa mapana zaidi—muitikio unaostahili katika hali ya dharura. Tunasifu hatua zote zilizokwisha chukuliwa hadi sasa. Sasa, hata hivyo, tunapenda kuchunguza kwa ukamilifu zaidi kile ambacho mwaka ujao unaweza kukihitaji. Jitihada zenu kuchochea maendeleo ya Mpango katika miezi yake ya mwishoni pasipo kuepukika zitabumbwa na jukumu lenu nyeti la kuwaongoza marafiki katika muitikio wao kwa janga la kiulimwengu linaloendelea kukunjuka . Mazingira haya ya kipekee yanahitaji kwamba tuwasemeshe ninyi moja kwa moja; mnaweza kuisambaza barua hii kwenye jumuiya zenu, kwa ujumla wake au sehemu zake kadhaa, kama mtakavyoona inafaa.

Tulipoelezea shauku yetu ya kuona programu elfu tano za ukuaji wa nguvu zikianzishwa ifikapo mwishoni mwa Mpango huu wa Miaka Mitano, tulifahamu fika kabisa juu ya ukubwa wa kazi ambayo hili lingemaanisha, lakini hali ya ulimwengu ilihitaji hili. Tulitoa wito kwa ajili ya kuchapuzwa kwa kazi ya uimarishaji wa programu za ukuaji kila mahali. Tulifurahishwa kuona jinsi wasaidizi wa Hoja walivyoamshika kwenye utendaji, wakiweka kiasi cha juhudi ambacho hakina kifani. Katika kipindi cha miaka minne jumuiya ya Kibahá'i imezidisha mara mbili yote mawili idadi ya shughuli za msingi zinazotokea kote ulimwenguni na idadi ya washiriki wao. Kuweza kuleta mamia kwa maelfu ya watu kwenye ukumbatiaji wa shughuli za jumuiya katika kipindi kifupi kama hicho ni maendeleo ya kiuwezo ambayo hayana ulinganisho katika Mipango yoyote iliyopita katika mlolongo wa sasa.

Mengi, basi, yametimizwa, na hiki ni kiashirio dhahiri cha nguvu na ujasiri wa jumuiya ya Kibahá'i. Lakini, kama ambavyo tayari mnambua, janga la sasa limebadilisha muktadha ambamo Mpango unatekelezwa. Tumefurahishwa kwa jinsi jumuiya nyingi zilivyopiga hatua za maendeleo makubwa na ya haraka katika kujirekebisha kufuatana na uhalisia huu mpya. Mbali na kukiona kipindi cha sasa kama mapumziko tu ya kulistahimiliwa kwa utulivu, zimetambua kwamba hali ya ulimwengu imesababisha haja ya kutoa huduma yenye tija kwa jamii ya binadamu kuwa ya haraka zaidi. Kwa kiuhalisia, shughuli zinazotekelezwa lazima zikidhi hali zilizopo, lakini pasiwe na shaka kwamba huu ni wakati kwa ajili ya shabaha bora, azma kuu, na jitihada shadidi (za

nguvu). Kama ifahamikavyo vyema, shughuli za Mpango zimekusudiwa kukuza ari ya kijumuiya inayositawi, ambayo kupitia hiyo ustahimilivu kwa changamoto kubwa pia huimarishwa. Jitihada za kielimu hulenga kuinua idadi ikuayo ya roho ambazo zinaweza kuchangia kwenye usitawi wa kiroho na kimwili wa jumuiya; mikutano ya ibada hulea moyo wa huduma kadiri inavyositawi, ikijikita mizizi katika utamaduni wa ibada ya pamoja. Kwa kifupi, uendelezaji wa Mpango humaanisha kujenga uwezo wa kutembea katika njia ya huduma wakati wote na kila msimu—ambao lazima kwa hakika ujumuishe nyakati za hatari kubwa katika maisha ya mwanadamu, kama ilivyo sasa. Ni muhimu, basi, kwamba hatua zinazochukuliwa kujifunza jinsi ya kutumia muundo wa utendaji wa Mpango kwa mazingira ya sasa ya ulimwengu ziendelee kwa bidii kubwa; kwa uwezekano wote, janga la kiafya la kiulimwengu litakuwa na athari ya moja kwa moja juu ya shughuli za Kibahá'i, kwa kiwango kikubwa au kidogo zaidi, kwa miezi au hata miaka, na kazi ya kujirekebisha kulingana na hali haiwezi kuahirishwa. Kuhusiana na hili, Washauri wa Bara na wasaidizi wao, wakiongozwa kwa ustadi mkubwa na Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, wameonesha dhamira inayochochea hisia za ndani katika jitihada zao kuwahimiza marafiki na kuwaelekeza katika mbinu zao kwa kazi iliyopo mbele yao; bila shaka watafanya vivyo hivyo kwa duru nne zijazo na zaidi.

Tunatambua, bila shaka, kwamba baadhi ya shughuli zililazimika zisitishwe, na mikakati au njia mahsusi ambazo hazifai kwa hali ya sasa zilibidi ziwekwe kando kwa muda. Hata hivyo, wakati uwezekano fulani fulani umefungwa kwa muda, mwingine umefunguka, na njia mpya zimeibuka kwa ajili ya uimarishaji wa mitindo ya sasa ya shughuli. Unyumbulikaji umethibitika kuwa wa thamani sana, lakini vivyo hivyo umakini wa kuhakikisha kuwa kimsingi tabia ya shughuli za mahali katika jumuiya hazichakachuliwi; juhudi za kulea jumuiya zinazoshamiri ndani ya ujirani na vijiji na katika klasta nzima lazima ziendelee. Kwa baadhi ya mazingira, hali za sasa zimetengeneza fursa ambazo hazikutarajiwa kwa ajili ya kupanua ushiriki wa jumuiya katika mikutano ya ibada na vikundi vya mafunzo, zikiendeshwa huku usalama ukiwa kwenye fikra. Wazazi wengi ambao familia zao zimezuiliwa kwenye mazingira ya nyumbani wamekaribisha msaada ambao umewasaidia kuhama kutoka kuwa watazamaji hadi kuwa wahusika wakuu katika elimu ya kiroho ya watoto wao. Vijana chipukizi na vikundi vya vijana wamegundua uwezo wa matendo rahisi ya huduma yenye huruma yafanywayo kwa hekima. Hata hivyo, ingeeleweka kama mkiamua, kwa baadhi ya mazingira, kwamba mipango inayohitaji kuhama kwa watangulizi, wakufunzi wasafiri au walimu watembezi itapaswa kuahirishwa, na hili lisiwape sababu ya kuwa na wasiwasi; mnaweza kutathmini upya hali itakavyokuwa miezi ya hapo mbele. Mpango ujao wa Mwaka Mmoja ungebeba fursa ya kutimiza malengo au mambo yoyote ambayo mwishowe yanaweza kubakia yasiyofikika katika Mpango wa sasa.

Tunatambua kwamba kuendelea kufanya kazi katika kipindi hiki cha majanga, kwa namna nyingi, kutawaweka katika mashaka ya kifedha, na dhiki ya kiuchumi inayopitiwa na wengi katika jumuiya inaweza kubinya rasilimali ambazo kwazo mnachota. Muwe na hakika kwamba tunasimama kidete kuwasaidia. Pasiwe na shaka wala utata wa kiuelewa katika jambo hili: ni muhimu kwamba asasi za Imani ziendeleze shughuli zao katika kipindi hiki chote na zisikwamishwe na ukosefu wa rasilimali katika kutekeleza majukumu yao ya kimsingi. Bila shaka, kundi lote la waaminifu katika kila nchi watakusanyika kuwazunguka, na hususan, tuna imani kwamba waumini wenye nyenzo watajitokeza kuwasaidia.

Kama mtambuavyo, kuna ukosefu mkubwa wa usawa kwa jinsi ambavyo jamii mbalimbali zinavyozikabili adha zitokanazo na janga hili; kwa sababu hiyo, changamoto ambazo zinayakabili Mabaraza mbalimbali ya Kitaifa hazifanani. Na changamoto hizi zitabadilika baada ya muda. Hii itahitaji uharaka na wepesi mkubwa mno kadiri asasi za mahali, za kanda, na za kitaifa zinavyotafuta kuusoma uhalisia wao na kuwa macho kwa maendeleo mapya. Tunapenda kushawishi fikra zenu kwamba ushirikiano wenu na Washauri utakuwa wa umuhimu mkubwa sana:unapaswa uwe wa kujidhatiti na endelevu, mabadilishano ya karibu kila mara ya taarifa na umaizi, kuhakikisha kwamba mnaitikia kwa haraka kwenye mahitaji ya jumuiya yenu, kutazamia matatizo kabla hayajaibuka, kunyaka fursa zinazofunguka, na kuunga mkono jitihada zinazoleta matumaini. Hatua zipi hasa zinapaswa kuchukuliwa na asasi za Kibahá'i kwa uhalisia itategemea na mazingira husika. Lakini kila mahali, marafiki watahitaji muongozo dhahiri na wa wakati; uangalifu maalum lazima utolewe kwa wale ambao wapo katika hatari zaidi ya kupata virusi vyenyewe, au kutokana na athari za kiuchumi za usambaaji wake; na njia za kiubunifu zitahitajika ili kudumisha moyo wa pamoja wa jumuiya katika nyakati za masahibu. Mitandao ya aina mbalimbali ikiundwa na familia, kaya za ujirani, au makundi mengine inatoa msaada wa thamani kwa wengi; muwe na imani na welekevu wa jumuiya zenu, na mtafute kuchota vipaji na nguvu zao kikamilifu. Kadiri ambavyo tayari hali imekuwa mbaya zaidi kwa baadhi ya sehemu, Mabaraza ya Kitaifa katika nchi ambazo hadi sasa zimeepushwa na madhara makubwa zaidi ya gonjwa hili lazima yakumbuke kwamba kuna uwezekano wa madhara makubwa zaidi kutokea, na maandalizi yoyote yanayoweza kufanywa sasa kwa ajili ya hatima hiyo, kabla vizuizi zaidi havijawekwa vitakavyokwamisha jitihada hizo, yanapaswa yaanze mara moja—bila kuibua hofu lakini bila kuchelewa. Mabaraza ya Kiroho ya Mahali hususan yanapaswa yafikirie ni njia gani zilizo ndani ya uwezo wao za kuzuia, kufariji, au kupunguza ukali wa mateso katika jamii pana ambayo kwayo wao ni sehemu yake.

Wakati jamii inapokuwa katika shida na mateso kama haya, wajibu wa Wabahá'i kutoa mchango wenye kujenga kwa ajili ya mambo ya binadamu huonekana wazi zaidi. Huu ni wakati ambapo mbinu tofauti tofauti lakini zinazohusiana za kiutendaji hukutana mahali pamoja, wakati mwito kwa ajili ya huduma hugonga kwa sauti. Mtu mmoja mmoja, jumuiya na asasi za Imani—wahusika wakuu wasioweza kutenganishwa katika uendelezaji wa ustaarabu—wana nafasi ya kuonesha sura mbalimbali za namna ya maisha ya Kibahá'i, wakijipambanua kwa ukomavu uongezekao katika utekelezaji wa majukumu yao na katika uhusiano wao mmoja kwa mwingine. Wanaitwa kuelezea kikamilifu zaidi uwezo wa Imani wa ujenzi wa jamii. Mawakala na miradi iliyowekwa wakfu kwa ajili ya vitendo vya kijamii wanaweza kurekebisha mbinu zao ili kukidhi mahitaji yaliyopanuka; jitihada za kufanya hili zina uhakika wa kuzijaza programu zinazoendelea maana na kusudi la ndani zaidi. Zaidi, michango ya Wabahá'i kwa mijadala inayoibuka upya katika jamii inatoa shauku ya hali ya juu, na kuna wajibu wa kujihusisha hapa vile vile. Wakati ambapo uharaka wa kufikia viwango vya juu zaidi vya umoja, ulioegemezwa juu ya ukweli usiopingika wa umoja wa jamii ya binadamu, unapokuwa dhahiri kwa idadi kubwa na kubwa zaidi, jamii huwa katika uhitaji wa sauti dhahiri ambazo zinaweza kuelezea kwa ufasaha kanuni za kiroho ambazo zimo katika hamu hiyo.

Bila shaka mnatambua daima kwamba wajibu wenu hufika mbali zaidi ya ule wa usimamizi wa masuala ya jumuiya na kuelekeza nguvu zake kwenye utimizaji wa malengo bora mnatafuta kuinua utambuzi wa zile nguvu za kiroho ambazo zipo kwa kila muumini aliyehakikishwa na ambazo lazima zielekezwe katika saa ya kuhitajika. Ni nguvu hizi hizi ambazo huijaalia jumuiya

uwezo wa kustahimili changamoto na kurejea kwenye hali yake ya kawaida kwa haraka, kuihakikishia uadilifu wake na kuendelea kuielekeza kwenye kazi yake maalum na takatifu ya kuhudumia jamii ya binadamu na kuinua muono wake wa siku za baadaye.

Haiwezekani kutabiri kiwango ambacho gonjwa hili litashawishi mjongeo wa kuelekea umoja miongoni mwa mataifa. Lakini hakuna shaka kwa vyovyote kwamba, kwa juhudi za jumuiya ya Kibahá'i, miezi iliyo mbele yetu ni yenye matokeo makubwa. Kwa hakika, ni nadra kwamba iwe vinginevyo. Mwaka huu wa mwisho, wa Mpango wa mwisho, katika mlolongo unaopelekea robo ya mwisho ya karne ya kuanza kwa Zama za Utungo, utahitimisha msingi ambao juu yake utawekwa mlolongo ufuatao wa jitihada za kiulimwengu. Ni kitendo kinachohitimisha katika mfululizo wa matukio ya kuvutia mno ambayo hatima yake bado haijulikani.

Haupiti muda ambapo hampo katika mawazo yetu. Imani na matumaini yetu yote katika uwezo wenu wa kukabiliana na changamoto hizi hutokana na utambuzi wetu kwamba muungaji mkono na msaidizi wa mwisho ni Uzuri wa Abhá Mwenyewe. Katika maombi yetu kwenye Vizingiti Vitakatifu, tunamsihi Yeye awafanye michirizi safi/mitakatifu kwa ajili ya utiririkaji wa rehema na neema Zake kwa jamii ya binadamu.

[Imesainiwa na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu]

Nakala: Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa
Bodi za Washauri
Washauri